**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**SHULE YA SEKONDARI MITEJA**

S. L. P 164

KILWA

…………………………….

KUMB. NA. MTSS/REG20/ ……..

JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………………………………………………………

S. L. P ……………..

KILWA

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MITEJA ILIOPO KATA YA MITEJA WILAYANI KILWA MKOA WA LINDI KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020:**

## 1: 0 UTANGULIZI:

Ninayofuraha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 20……katika shule ya sekondari Miteja.HONGERA SANA

Muhula wa masomo utaanza ………………………..hivyo unatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo mara moja ili kuanza masomo. Kumbuka serikali imeshatumia fedha nyingi kugharamia elimu yako.

## 2:0 MAANDALIZI MUHIMU YA KUKAMILISHA:

### 2:1 SARE ZA SHULE - WASICHANA:

**Sketi** mbili ndefu **rangi ya kijani** zenye marinda ya kawaida, **Hijabu** mbili nyeupe ya mikono mirefu au **Mashati** mawili meupe ya mikono mifupi, **Viatu vyeusi** jozi mbili visivyo na kisigino kirefu (high heel), **Soksi** jozi mbili za rangi nyeupe, **Trak suti** ya rangi ya bluu kwa ajili ya michezo shuleni pamoja na **Raba** nyeupe.

### 2:2 SARE ZA SHULE - WAVULANA

**Suruali** mbili za **rangi ya kaki** zisizo za kubana (modo), **Mashati** mawili meupe ya mikono mifupi, **Viatu vyeusi jozi mbili** vya kufunga kwa kamba jozi mbili, **Soksi** jozi mbili za rangi nyeupe, **Bukta** na **T-Shirt** nyekundu kwa ajili ya michezo shuleni, **T-Shirt** moja rangi ya bluu yenye nembo ya shule itakayo valiwa siku ya Jumatano na Ijumaa. Inapatikana shuleni kwa kulipia

### 2:3 VIFAA VINGINE KWA WAVULANA NA WASICHANA :

(i) Uje na **Daftari** 9 kubwa counter book za masomo. Daftari 3 za msomi, **Kalamu** za ragi ya bluu au nyeusi kwa ajili ya kuandikia. **Faili** moja kwa ajili ya kutunzia kumbukumb binafsi za mwanafunzi na mkebe wa hesabu.
(ii) Uje na vifaa vya kufanyia usafi shuleni **Ufagio** wa chelewa wa wima.
(iii) Uje na **Jembe** lenye mpini na **Fyekeo j**ipya lililonolewa siku utakayokuja katika usajili.
(iv) **Rem** moja ya karatasi.

## 3:0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria **Na. 5** ya elimu ya mwaka **1978** iliyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka **1995**. Aidha shule inazingatia miongozo yote iliotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi pamoja na wizara ya 0FISI YA RAIS- TAMISEMI yenye dhamana ya usimamizi na uendeshajiwa elimu.

**3:1 MAMBO KADHAA YA LAZIMA YA KUZINGATIA UKIWA KAMA MWANAFUNZI:**

i. Kuheshimu viongozi, wazazi , wafanyakazi wote wa shule, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla.
ii. Kujituma muda wote katika masomo kwani ndio lengo kuu la wewe kufika hapa shuleni.
iii. Mahudhurio mazuri ya shule **tabia ya utoro haivumiliki kabisa.**
iv. Kuwahi katika kazi /shughuli zote ndani na nje ya shule na kutunza vifaa/mali za umma.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu ya maelekezo utakayo pewa ukiwa kama mwanafunzi.
vi. Kujali, kutunza na kuzingatia wakati wote usafi mazingira ya shule mavazi na usafi wa mwili ***( epuka kunyoa au kusuka mitindo isiyokubalika shuleni)***.
vii. Kuzingatia ratiba muda wote. kujali na kuheshimu kengele ikiwemo kengele ya dharura.
viii. Unatakiwa kuwa mfano wa kuigwa kwa kuwa na tabia njema.

**3:2 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA**

i. Wizi
ii. Ubakaji, Uasherati (kuwa katika mahusiano ya kimapenzi) na ushoga au usagaji.
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvitaji wa bangi, kutumia cocaine na mirungi. Pia uvutaji wa sigara hauruhusiwi.
iv. Kupiga au kupigana.
v. Kuharibu kwa mkusudi mali ya umma/shule.
vi. Kudharau bendera au wimbo wa taifa.
vii. Kuoa au kuolewa na Kusababisha mimba au kuwa na mimba.
viii. Kugoma , kuchochea ,kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
ix. Kukataa/kugomea adhabu kwa makusudi au Kupatikana na kosa lolote la jinai.
x. Kushiriki katika kumbi za starehe, vigodoro, disko na michezo isiyokubalika kama kamari.
xi. Kuwa na simu ya mkononi shuleni.

**4:0: MAMBO YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI SIKU YA USAJILI WA MWANAFUNZI.**

**Medical examination form** ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa shuleni mara utakaporipoti shuleni

Utajaza form ya **mkataba wa kuboresha wa elimu.** Mkataba huo utamuhusisha mwanafunzi, mzazi/mlezi wake, mwenyekiti wa bodi ya shule , mkuu wa shule na afisa mtendaji kata. Ni muhimu kuusoma vizuri na kuuelewa.

**5:0 AGIZO MUHIMU**

Siku ya tarehe **03/01/2020** kutakua na kikao cha wazazi wa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza miteja sekondari. Agenda kuu ni kupeana maagizo muhimu. ***Tafadhali fika bila kukosa.***

**Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na**

***0784 541 834 mwalimu wa taaluma***

***0785 038 535 makamu mkuu wa shule***

***HONGERA SANA KWA KUCHAGLIWA - KARIBU SANA MITEJA SEKONDARI***

**…………………………..**

**SELEMANI M. MSOFE**

**MKUU WA SHULE- MITEJA SEKONDARI**

**0784900766**

**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**

**SHULE YA SEKONDARI MITEJA**

**TAARIFA YA MAENDELEO YA MWANAFUNZI KIMASOMO (TAALUMA) NA TABIA**

JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………… KIDATO CHA ……………
MUHULA WA ………………………  MWAKA …………………………….
A: TAALUMA

| **SOMO** | MAZOEZI | MAJARIBIO | JUMLA | WASTANI | DARAJA | NAFASI | MAONI | SAINI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **CIVICS** | | | | | | | | |
| **KISWAHILI** | | | | | | | | |
| **ENGLISH** | | | | | | | | |
| **GEOGRAPHY** | | | | | | | | |
| **HISTORY** | | | | | | | | |
| **CHEMISTRY** | | | | | | | | |
| **BIOLOGY** | | | | | | | | |
| **MATHEMATICS** | | | | | | | | |
| **PHYSICS** | | | | | | | | |
| JUMLA | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |

AMEPATA DIVISION …………………NA AMESHIKA NAFASI YA ………………….. KATI YA WANAFUNZI…………… WALIOFANYA MTIHANI.

Maoni ya mwalimu wa darasa

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………

**B: TABIA NA MWENENDO**

| **TABIA NA MWENENDO** | **DARAJA** | **MAONI** |
|---|---|---|
| TABIA KWA UJUMLA | | **Nzuri Sana - Nzuri - Wastani - Dhaifu - Mbaya** |
| BIDII KATIKA KAZI NA MASOMO | | **Nzuri Sana - Nzuri - Wastani - Dhaifu - Mbaya** |
| NIDHAMU KWA UJUMLA | | **Nzuri Sana - Nzuri - Wastani - Dhaifu - Mbaya** |
| USAFI BINAFSI NA MAZINGIRA | | **Nzuri Sana - Nzuri - Wastani - Dhaifu - Mbaya** |
| UTII WA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE | | **Nzuri Sana - Nzuri - Wastani - Dhaifu - Mbaya** |

MAONI YA MWALIMU WA TAALUMA

…………………………………………………………………………………………………………………………………………………..

**MAAGIZO MUHIMU**

Shule imefungwa leo **06** mwezi **12** mwaka **2019** na itafunguliwa **06** mwezi **01** mwaka **2020**

Kila mwanafunzi wa kidato cha mtihani (kidato cha **II** na **IV-**2020) anatakiwa kuchangia **REM MOJA** ya karatasi kwa ajili ya mazoezi ya kujiandaa na mitihani yake ya taifa. Pia kutakua na **kambi ya masomo** kwa wanafunzi wa vidato hivyo utaratibu na gharama utaelekezwa kwenye vikao vya wazazi wa wanafunzi husika.

**……………………………**

**SELEMANI M. MSOFE**

**MKUU WA SHULE**